**12 JUNI, 2024**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Arobaini na Sita – Tarehe 12 Juni, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU:**

**MWENYEKITI:** Maswali, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Nimwite sasa Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 592

**Uhaba wa Walimu wa Kike na wa Sayansi Songwe**

**MHE. JULIANA D. SHONZA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza tatizo la uhaba wa walimu wa kike katika shule za msingi na walimu wa sayansi katika shule za sekondari Mkoani Songwe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Katimba kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Songwe una shule za msingi za Serikali 481 na walimu wa shule za msingi 4,211, kati yao walimu 1,932 ni wa kike na 2,279 ni wa kiume. Kuanzia mwaka 2021/2022 hadi 2022/2023 Mkoa wa Songwe ulipangiwa walimu 570 kati yao 272 wa shule za msingi na 298 wa shule za sekondari. Aidha, kati ya walimu 298 wa sekondari, walimu 86 ni wa masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa walimu wa kike katika malezi ya wanafunzi pamoja na uhitaji wa walimu wa masomo ya sayansi. Katika kutatua changamoto hizo, katika mwaka 2023/2024 Serikali inatarajia kuajiri walimu 12,000 wa kike na wa kiume wa masomo yote yakiwemo ya sayansi ambao watapangiwa vituo mbalimbali ikiwemo na Mkoa wa Songwe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Juliana Shonza, swali la nyongeza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, pia nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Songwe ni mpya na katika kipindi cha Awamu ya Sita tumepata shule nyingi sana za msingi pamoja na sekondari ikiwemo shule ya wasichana ambayo ina-*deal* na mchepuo wa sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa tuliyonayo katika Mkoa wa Songwe ni upungufu mkubwa sana wa walimu hasa walimu wa masomo ya sayansi ambapo kitakwimu kwa walimu wa shule ya msingi, upungufu ni 3,077 na sekondari ni walimu 366.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitakuwa na swali la nyongeza, lakini nataka tu nitoe ombi kwa Serikali kwamba katika huo mgao ujao ninaomba sana waweze kutoa kipaumbele kwa Mkoa wa Songwe kulingana na upungufu mkubwa wa walimu tulio nao, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, ametoa ombi, nimekuona Mheshimiwa Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Msingi Kimenye ina walimu wawili tu wa kike, je, Serikali iko tayari kupeleka walimu wengine wa kike ili kuweza kuwasaidia watoto wa kike wanaosoma katika shule hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kupambania haki ya watoto kupata elimu, lakini kuwapambania watoto wa kike waweze kupata walimu wa kike kwa ajili ya malezi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kujibu katika majibu ya msingi kwamba Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa walimu wa kike katika malezi ya wanafunzi. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kutazama mahitaji ya uhitaji wa walimu ikiwemo walimu wa kike kwa ajili ya kuwapeleka katika shule zetu hizi waweze pamoja na kufundisha, lakini kuwa walezi kwa watoto wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali itatizama na katika vipaumbele na sifa za kuajiri walimu na kuwapeleka katika shule na kwa kuzingatia mahitaji itaendelea kupeleka walimu kwa sifa mbalimbali ili kuhakikisha kwamba wanaenda kuwa walezi pia kwa watoto wa kike. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakunda, nimekuona.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tatizo la walimu wa kike hasa kwenye shule za vijijini ni kubwa mno na inafikia wakati ambapo kuna shule zinakosa mwalimu hata mmoja wa kike jambo ambalo wanafunzi wa kike wanakosa *matron* kwenye shule.

Je, Serikali haioni upo umuhimu sasa wa kuangalia mgawanyo wa walimu wa kike katika nchi hii ili kuhakikisha kwamba walimu wa kike wanaongezwa zaidi katika shule za vijijini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taratibu, waajiri wa walimu kimsingi unazingatia taaluma. Kwa hiyo, ajira zile za walimu zinazingatia *professionalism,* lakini hoja ya Mheshimiwa Mbunge ni hoja ya msingi sana na sisi kama Serikali tumeipokea kwa ajili ya kuichakata na kuangalia namna nzuri ya kuweza kufanya utekelezaji kwa maana ya kuzingatia uhitaji wa walimu wa kike katika shule zetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali linalofata. Nimwite sasa Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, Mbunge wa Sumve aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Justin Nyamoga.

Na. 593

**Ujenzi wa Shule ya Sekondari Kata ya Malya – Sumve**

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA K.n.y. MHE. KASALALI E. MAGENI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Shule ya Sekondari Kata ya Malya, Kitongoji cha Mwashilibwa ili kuongeza huduma Vijiji vya Mwitemba, Talaga na Kitunga?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari *(SEQUIP)* inaendelea na ujenzi wa shule za sekondari kwenye maeneo ya kata yasiyo na shule na maeneo yenye msongamano wa wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa shule ya sekondari ya mikondo miwili kupitia Mradi wa *SEQUIP* awamu ya tatu katika Jimbo la Sumve unatekelezwa katika Kata ya Malya, Kijiji cha Kitunga. Serikali itaendelea kujenga shule katika maeneo yasiyo na shule ili kuwarahisishia wanafunzi kupata elimu katika mazingira ya karibu na nyumbani kwao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Justin, kwa niaba ya Mheshimiwa Kasalali, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, swali la kwanza ni kwamba ni kweli kuna utaratibu wa shule za *SEQUIP* kujengwa na mojawapo ikiwa ni katika Jimbo la Mheshimiwa Kasalali, je, ni lini kwa mwaka huu wa fedha shule hizo zitaanza kujengwa kwenye jimbo hili na majimbo mengine? *(Makofi)*

Swali la pili, kuna shule za *SEQUIP* za awamu ya kwanza ambazo hazikuwa zimekamilika, je, ni lini Serikali itapeleka fedha ili kukamilisha shule hizo kwenye majimbo yote ikiwemo Jimbo la Sumve na Jimbo la Kilolo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alitafuta fedha na akapata fedha jumla ya shilingi trilioni 1.2 katika mradi tunaouita Mradi wa *SEQUIP* ambao lengo lake ni kuongeza shule zetu za sekondari kwenye kata na kuhakikisha zinafika, tunaongeza idadi ya shule kwa ajili ya kupunguza kwanza umbali wa wanafunzi kusafiri ili kufika kwenye shule, lakini pia kupunguza msongamano katika baadhi ya maeneo ambayo kuna msongamano kwenye shule hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa lengo la Serikali na lengo la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha anaboresha sekta ya elimu na hasa elimu hii ya shule za sekondari na shule za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Mbunge ameuliza kwamba ni lini awamu hii au mwaka huu fedha zitatolewa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa shule hizi katika mwaka huu wa fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Serikali imeshafanya uhakiki wa maeneo yote yaliyoainishwa kwa ajili ya ujenzi wa shule hizi za kata katika mwaka huu na ninamhakikishia, wakati wowote fedha zitatolewa kwa ajili ya kuhakikisha tunatekeleza mradi huu kwa kadiri vile tulivyokuwa tumepanga kwa maana ya awamu ya mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, Mheshimiwa Mbunge ametaka kufahamu kwamba zile shule za awamu ya nyuma ambazo hazikukamilika, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kuhakikisha inakamilisha shule hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Serikali ilishaanza kutoa fedha na itahakikisha inapeleka fedha ili kukamilisha ujenzi wa miundombinu muhimu ya shule hizi za kata ili wanafunzi waweze kuanza kuzitumia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea, nimwite sasa Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini, sasa aulize swali lake.

Na 594

**Kusawazisha Vilima kwenye Barabara ya Ninde, Kala na Wampembe - Nkasi**

**MHE. VINCENT P. MBOGO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itasawazisha vilima vilivyopo kwenye Barabara ya Ninde, Kala na Wampembe ambavyo vimekuwa vyanzo vya ajali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, vilima vilivyopo katika barabara ya Namanyere – Kakoma – Ninde vimeanza kufanyiwa kazi kwa kupunguza miinuko mikali na kuweka tabaka la zege lenye urefu wa meta 150 kwa gharama ya shilingi milioni 84.75 katika mwaka 2022/2023. Aidha, katika mwaka 2023/2024 Serikali imetenga shilingi milioni 550 kwa ajili ya kupunguza vilima na kujenga tabaka la zege lenye urefu wa meta 700 katika Barabara ya Kitosi - Wampembe ili kuondoa maeneo yote korofi ambapo mkandarasi ameanza kazi.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2024/2025 shilingi milioni 475 imetengwa kupitia Mfuko wa Jimbo kwa lengo la kuvisawazisha vilima vilivyopo katika Barabara ya Nkana – Kala. Aidha, Serikali imepanga kutumia shilingi milioni 180 katika bajeti ya mwaka 2024/2025 kwa ajili ya kupunguza miinuko mikali iliyobaki kwa kujenga tabaka la zege lenye urefu wa meta 200 hivyo kumaliza kabisa tatizo lililopo kwenye vilima vya Barabara ya Namanyere – Kakoma – Ninde.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbogo, maswali ya nyongeza.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi, nina swali moja la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itajenga Barabara ya Kizumbi – Lupata hadi Msamba kwani kuna shule mpya ya sekondari imejengwa na ni eneo la kiuchumi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kujibu kwenye majibu ya msingi, Serikali tayari imeshaanza kufanya ujenzi wa barabara mbalimbali katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuhudumia barabara katika jimbo lako, pia ikiwemo

barabara hii ya Kizumbi mpaka kufika Msumba. Nakuhakikishia barabara hiyo itajengwa na Serikali italeta fedha kwa ajili hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Bado tunaendelea na maswali kwa TAMISEMI, namwita sasa Mheshimiwa Boniphace Nyangidu Butondo, Mbunge wa Kishapu, aulize swali lake.

Na. 595

**Hitaji Vituo vya Afya – Tarafa ya Negezi Kishapu**

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga vituo vya afya katika Tarafa ya Negezi ili kuboresha huduma za afya kwa wananchi kwani tarafa hiyo ina kituo kimoja tu cha afya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarafa ya Negezi ina kata nane ambapo kata mbili kati ya hizo zina vituo vya afya. Vituo hivyo ni Kituo cha Afya Negezi kilichopo Kata ya Negezi ambacho kilipokea shilingi milioni 500 mwaka 2021/2022 na Kituo cha Afya Nhobola kilichopo Kata ya Talaga ambacho ni cha muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya kwenye kata za kimkakati kote nchini zikiwemo kata zitakazokidhi vigezo katika Tarafa ya Negezi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, kwanza naomba niipongeze Serikali kwa ujenzi wa Kituo cha Afya cha Negezi ambacho kimeanza kufanya kazi sasa, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, Kituo cha Afya cha Mwanhakanga, Kituo cha Afya cha Mwamigumbi na Kituo cha Afya cha Dulisi, ni vituo vya afya ambavyo vimejengwa kwa nguvu za wananchi na michango iliyotokana na mapato ya halmashauri.

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba inakamilisha miundombinu iliyosalia ikiwemo wodi za akinamama, akinababa na watoto, *walkways, fence* na mambo mengine yanayoendana na sifa za vituo vya afya ili mradi vituo vile vianze kufanya kazi kikamilifu na ipasavyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Zahanati ya Lagana ni moja kati ya zahanati ambazo zinahudumia kata tatu zinazozunguka katika maeneo hayo na moja kati ya mambo ambayo tulielekezwa na Serikali kama Waheshimiwa Wabunge ni kutoa mapendekezo ya kuhakikisha maeneo ambayo ni ya kimkakati na yaliyopembezoni yaweze kupewa kipaumbele cha kuwekewa vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini mpango wa Serikali katika kuhakikisha zahanati hii inapandishwa hadhi kuwa *health center* ili kiweze kuhudumia maeneo haya yanayozunguka kata jirani? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa ya kuwatetea wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la kwanza Mheshimiwa Mbunge ametaka kufahamu kuhusu Kituo cha Afya cha Mwanhakanga, Kituo cha Afya cha Dulisi na Mwagimbi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya cha Mwanhakanga tayari kimekamilika na kimeanza kutoa huduma, lakini Kituo cha Afya cha Dulisi na Kituo cha Afya cha Mwagimbi ni vituo vya afya ambavyo pia vimejengwa kwa nguvu za wananchi na vina

majengo ya *OPD* pekee. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tayari imeshatenga fedha kwa ajili ya miradi viporo ya hospitali, lakini mahsusi pia kwa ajili ya miradi viporo ya vituo vya afya. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Serikali itakuja kukamilisha ujenzi wa vituo vyake hivi muhimu vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili la Mheshimiwa Mbunge kuhusu Zahanati hii ya Lagana, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inafanya jitihada ya kupata fedha ili Zahanati hii ya Lagana iweze kupandishwa hadhi kuwa kituo cha afya kutokana na umuhimu wake na kutokana na hoja ya msingi ambayo Mheshimiwa Mbunge ameieleza kuhusiana na kupatikana kwa kituo cha afya kwenye eneo alilolitaja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Minza Mjika, nimekuona.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Binza ni Kata kubwa sana na ina wakazi 9,787 lakini haina kituo cha afya, je, lini Serikali itajenga kituo cha afya katika kata hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI alishazungumza na Waheshimiwa Wabunge na akawa amewataka waweze kuainisha vituo vya afya vya kimkakati vya kujengwa katika maeneo yao. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa kama Kata ya Binza ni miongoni mwa kata zinazohitaji vituo vya afya vilivyoainishwa kimkakati kwenye maombi yale yaliyoelekezwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, ninamhakikishia kwamba Serikali inatafuta fedha ili kukakikisha vituo hivyo vya afya vinajengwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Dkt. Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Kata ya Didia iliyopo katika Jimbo la Solwa ni kata ambayo ina watu wengi zaidi ya 60,000.

Je, nini mpango wa Serikali kuwapatia kituo cha afya katika ksata hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali ni kuhakikisha inaimarisha huduma za afya msingi na katika kufanya hivyo imekuwa ikiboresha miundombinu ya hospitali za wilaya, vituo vya afya mpaka zahanati na namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali inaendelea na jitihada za kuhakikisha inapata fedha kwa ajili ya kuimarisha huduma ya afya msingi. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali itaendelea kutafuta fedha ili ije iweze kufikia ujenzi wa kituo cha afya katika Kata hii ya Didia kama ulivyosema ina wananchi wengi na wanahitaji huduma iliyo bora ya afya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Kimei, halafu utafuata Mheshimiwa *Engineer* Chiwelesa, *then* Mheshimiwa Omari Kigua.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, mwaka 2020 tulivyokuwa tunafanya kampeni, Serikali ilipandisha hadhi Kituo cha *OPD* Himo kuwa kituo cha afya na kutuahidi kwamba wangetupa majengo ya maabara, wodi moja pamoja na *mortuary*. Mpaka leo hii hakuna kilichofanyika lakini kituo kinaendelea kutoa huduma kama kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Serikali sasa iseme kwamba ni lini itatoa fedha kwa ajili ya majengo haya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti,

kwa hoja hii muhimu ya Mheshimiwa Mbunge naomba tukae baada ya kipindi hiki cha maswali na majibu ili tutazame mkwamo upo eneo gani. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba huduma za afya msingi zinaimarika na zinakuwa bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa misingi ya alichokisema Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tuna kituo ambacho kinatoa huduma ya kituo cha afya, lakini haina miundombinu ya msingi ya kuweza kutosheleza kutoa huduma ya kituo cha afya, nadhani kuna hoja ya msingi. Kwa hiyo, tutakaa na Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kuona changamoto ipo wapi ili Serikali iweze kupeleka fedha kwa ajili ya kuleta miundombinu muhimu katika kituo hicho cha afya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, katika bajeti hii ambayo tunaendelea nayo Serikali ilitenga shilingi bilioni nane kwa ajili ya ukarabati wa vituo vya afya takribani 20 ambavyo havitoi huduma kama vituo vya afya kamili na miongoni mwa vituo hivyo Wilaya ya Biharamulo tulitengewa shilingi milioni 500 kwa ajili ya kukarabati Vituo vya Afya vya Nyabusozi na Kalenge, lakini mpaka sasa pesa hiyo haijatoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kauli ya Serikali kwa sababu mwaka wa fedha unaisha na sijaona pesa hiyo ikiwa imepelekwa? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kujibu awali, lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba inaboresha huduma za afya msingi. Kwa hoja ya Mheshimiwa Mbunge, nimhakikishie kwamba Serikali ipo kazini na ndiyo maana kwanza ilianza kutenga bajeti. Kwa hiyo mimi na yeye tutakaa na tutazungumza tuone mkwamo upo sehemu gani.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Omari Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, Kata ya Jaila tunayo zahanati ambayo ina sifa zote za kuwa kituo cha afya, lakini kwa bahati mbaya kuna baadhi ya majengo hayajakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Mheshimiwa Naibu Waziri upo tayari kutuletea kiasi cha fedha kumalizia majengo hayo na kuwa kituo cha afya? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikifanya jitihada za kuboresha huduma za afya msingi. Katika jitihada hizo imekuwa ikipandisha hadhi zahanati kuweza kutoa huduma za vituo vya afya kwenye maeneo ambayo yanauhitaji, lakini yana mazingira ambayo yanawezesha kuanzishwa kwa kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ametaja eneo hili la Zahanati ya Jaila ambayo imepandishwa hadhi kuwa kituo cha afya. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali inatafuta fedha kuhakikisha hizi zahanati zote ambazo zimepandishwa hadhi kuwa kituo cha afya zinapatiwa fedha ili kuimarishwa ili huduma zitakazotolewa ziendane na huduma zinazotakiwa kutolewa katika vituo vya afya. Kwa hiyo, nikutoe shaka Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali inalifanyia kazi suala hili.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tumalizie swali la mwisho la Wizara hii. Nimwite Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, sasa aulize swali lake.

Na. 596

**Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Chunya**

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE K.n.y. MHE. MASACHE N. KASAKA** aliuliza:-

Je, ni lini ahadi ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Chunya itaanza kutekelezwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya unaendelea katika eneo la hospitali ilipo kwa kuiongezea miundombinu muhimu iliyokuwa imepungua. Serikali katika kipindi cha mwaka 2020/2021 hadi 2023/2024 imepeleka shilingi bilioni 2.5 ambapo majengo 13 yamejengwa yakijumuisha jengo la *OPD*, jengo la kuhudumia wagonjwa wa dharura *(EMD)*, jengo la maabara, jengo la kliniki ya mama na mtoto, jengo la upasuaji, wodi ya wazazi, jengo la stoo ya kutunzia dawa, wodi nne za kulaza wagonjwa, jengo la mama ngojea, jengo la kufulia na njia za kutembelea wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majengo yote haya yamekamilika na yanatumika. Katika mwaka 2024/2025 Serikali imetenga shilingi milioni 450 kwa ajili ya ujenzi wa uzio katika Hospitali ya Wilaya ya Chunya.

**MWENYEKITI:** Kwa niaba ya Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mheshimiwa Ally Mlaghila.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Chunya wanaishukuru sana Serikali ya Chama Cha Mapinduzi chini ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo imefanyika mpaka sasa, lakini wana maswali.

Je, sasa hizi pesa ambazo zimetengwa ni kweli zitawahi ili zipelekwe na hospitali hiyo kuanza kufanya kazi kwa haraka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, hospitali mojawapo katika Mkoa wa Mbeya ambayo ni kongwe sana ni Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Kyela. Je, ni lini ukarabati wa hospitali hiyo kwa viwango vya kimataifa utaanza kufanyiwa kazi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye majibu ya msingi katika mwaka 2024/2025 Serikali imetenga shilingi milioni 450 kwa ajili ya ujenzi wa uzio katika Hospitali ya Wilaya ya Chunya. Kama vile ambavyo tayari katika miaka ya nyuma Serikali ilikuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kuboresha na kukamilisha miundobinu katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya hivyo hivyo katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imetenga fedha na fedha zitafika kwa wakati kwa ajili ya kukamilisha mradi huo.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Flatei Massay.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi, Hospitali ya Halmashauri ya Mbulu imeanza kujengwa na karibu inamalizika lakini haitoi huduma kwa sababu shilingi milioni 500 za mwisho ilikuwa zipelekwe na mpaka sasa hazijapelekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, lini mtapeleka ile fedha shilingi milioni 500 ili hospitali ile ikaisha na wananchi wakapewa huduma ambayo wanastahili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha ujao Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kukamilisha miradi viporo ya hospitali za halmashauri. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hospitali ya kwao ya Halmashauri ya Mbulu na yenyewe itakuwa miongoni mwa hospitali zitakazohudumiwa kwa maana ya kukamilisha miundombinu ya hospitali ile iliyokuwa imebakia kwa sababu fedha imetengwa katika mwaka ujao wa bajeti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, nilikuona.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, Kijiji cha Kisana tunajenga zahanati ambayo imetumia zaidi ya miaka 10 haijakamilika. Ni lini Serikali itatoa hela ya kumalizia hilo boma? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitenga fedha kila mwaka wa bajeti kwa ajili ya kuhakikisha inakamilisha miundombinu ambayo haijakamika kwenye vituo vyetu vya kutoa huduma ya afya msingi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali imetenga bajeti, pia itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuhakikisha inaendelea kukamilisha miundombinu ambayo haijakamilika kwenye vituo vyetu vya kutoa huduma ya afya msingi ikiwemo katika zahanati hii katika Kijiji cha Kisana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Midimu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Hospitali ya Wilaya ya Itilima haina uzio, je, ni lini Serikali itaoa fedha za kujenga uzio ule? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikijenga miundombinu katika vituo vyetu vya kutolea huduma za afya msingi kwa kutumia utaratibu kwa fedha kutoka Serikali Kuu, lakini kwa kutumia fedha kutoka kwenye mapato ya ndani ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu huo Serikali itaendelea kuhakikisha inaboresha miundombinu ya vituo vyetu hivi vya kutolea huduma ya afya msingi. Kwa muktadha huo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba uzio katika hospitali

ya halmashauri aliyoitaja itaendelea kutafutiwa fedha, kutengewa fedha na kujengwa kwa utaratibu wa fedha kutoka Serikali Kuu, lakini kupitia pia mapato ya ndani ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunakwenda sasa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Nimwite sasa Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Kibamba, aulize swali lake.

Na. 597

**Madeni ya Watumishi wa Umma**

**MHE. ISSA J. MTEMVU** aliuliza: -

Je, hadi sasa Serikali ina madeni kiasi gani ya watumishi wa umma yanayohusu likizo, uhamisho na kusafirisha mizigo baada ya kustaafu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri nikuite, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete endelea.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Kibamba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2024 madeni ya watumishi wa umma yaliyohakikiwa na kukidhi vigezo vya kulipwa yanayohusu likizo, uhamisho na kusafirisha mizigo baada ya kustaafu yalikuwa na jumla ya shilingi bilioni 285.1. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 jumla ya madeni yenye ujazo wa shilingi bilioni 55.9 yamelipwa. Aidha, Serikali

itaendelea kulipa madeni ya watumishi yasiyo ya kimshahara kila mwaka kwa kuzingatia taarifa ya uhakiki wa madeni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issa Mtemvu, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ningeomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, Serikali inasimamiwa na Mwongozo wa Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2009 zinazotaka madeni ya watumishi wa umma yanapotokea tu yalipwe ndani ya miezi 12. Je, ni lini Serikali itasimamia mwongozo huu wa kikanuni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa madai mengine ya wazabuni na wakandarasi yanapochelewa kulipwa hulipwa na riba. Je, Serikali haioni haja sasa ije na sera na sheria hapa Bungeni ili iweze kuweka hiyo nafasi ya kuchelewa kulipa itawalipa na riba watumishi wa umma ili hiyo haja ya kuwalipa iende kwa kasi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo unaozungumzwa na Mheshimiwa Mbunge wa mwaka 2009 ni mwongozo unaohusu udhibiti wa ongezeko la madeni ya Serikali kwa watumishi wa umma. Ni kweli maneno kama anayosema Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ilieleza kwamba pamoja na mazingatio mengi ambayo yameelezwa ndani ya mwongozo huu, lakini moja ya jambo la msingi kabisa ni kuhakikisha kwamba Serikali inakuwa na mpango mzuri kwa ajili ya kurithisha madaraka na mara nyingi huo mwongozo unafanywa kwa kupitia bajeti zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika swali lake la kwanza kwamba Serikali inaendelea kusimamia mwongozo huu na pale ambapo panatokea mapungufu Serikali kupitia Ofisi ya Katibu Mkuu - Utumishi

imekuwa inapeleka maelekezo na kuendelea kukumbusha juu ya wale maafisa uajiri kuendelea kusimamia mwongozo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, madeni haya yanalipwa lini? Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imejipanga vizuri. Nataka nikutoe wasiwasi wewe, lakini pia kulitoa wasiwasi Bunge lako kwamba Serikali inaendelea kusimamia mwongozo huu na kuhakikisha kwamba madeni yote yale ambayo yamehakikiwa na taarifa zake zimeletwa katika mamlaka husika kwa ajili ya malipo, tunafanya hivyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika Mkoa wetu wa Iringa ulifanya ziara na hii changamoto ilijitokeza karibu katika wilaya zote za Mkoa wetu wa Iringa na wafanyakazi kwa kweli wanapata shida sana kwa sababu wanashindwa hata kutafuta nyumba nyingine kwa ajili ya kuhamia na wengine wameshindwa kusafirisha mizigo yao kule ambapo inatakiwa waende ambapo wameshastaafu.

Je, ni kwa kipindi gani anatakiwa adai haya madai yake kwa sababu yanakuwa yanachukua muda mrefu kiasi kwamba wanapata mateso makubwa sana? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kipindi gani mfanyakazi anatakiwa kudai madeni haya? Jambo la msingi narudia tena kwamba mwongozo wa mwaka 2009 umeelekeza waajiri wote kwamba kabla hamjapandisha watu madaraja, kabla mtu hajastaafu ni vyema mwongozo huu ukafuatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo upo wazi kabisa ambao unaelekeza nini kifanyike kabla hatujafika kwenye kudai madeni. Kipindi gani madeni haya yanatakiwa kulipwa? Nataka

nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba madeni haya yanatakiwa yadaiwe muda wowote ambao mtu anastahiki kulipwa stahiki zake kwa mujibu wa mwongozo ambao umetolewa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Simbachawene.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini nimedhani nisimame kwa ajili ya kutoa maelezo ili Waheshimiwa Wabunge walielewe jambo hili na Watanzania pamoja na watumishi walielewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni yanagawanyika katika namna mbili; yapo madeni yanayotokana na lolote linalotokea katika suala la mishahara. Haya yanahusika kabisa na Wizara ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, lakini madeni ambayo yanatokana na mambo mengine yasiyo ya mshahara kama vile uhamisho, masuala ya kusafirisha mizigo baada ya kustaafu, lakini pia na likizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni ya namna hii yanahusika na mwajiri au sekta husika. Sasa mwajiri anayezalisha madeni mengi sana ya namna hii ni Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambapo Waheshimiwa Wabunge sisi tupo kule kwenye mamlaka zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa kwanza kuomba ombi moja; ajenda zinapozungumzwa kwenye Kamati ya Uongozi na Fedha kule, moja kati ya vitu Waheshimiwa Wabunge tuwe tunahoji kule ni je, madeni haya ya watumishi yanayohusisha kusafirisha mizigo, masuala ya likizo na masuala ya uhamisho ni kiasi gani yanadaiwa? Kwa sababu kule ndipo ambapo yanazalishwa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge nimesema niliseme hili ili na sisi wenyewe tukishughulika kule tutapunguza huu mzigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Serikali ya Awamu ya Sita imeingia madarakani imejitahidi sana kulipa madeni haya.

Tumelipa jumla ya shilingi 167,980,000,000 lakini bado mzigo unazidi kuongezeka kwa sababu kule kwenye kuzalisha madeni bado kuna uzembe uzembe unatokea kwa sababu kila mwajiri huwa anatenga bajeti kwa ajili ya kushughulikia masuala haya ya uhamisho, likizo na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo inakuwa kwa nini sasa hayalipwi ni pale ambapo nadhani Waheshimiwa Wabunge tukienda kusimamia kule tunaweza tukasaidia watumishi wetu wakawa hawadai, lakini pia Serikali nayo ikawa haidaiwi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa George Simbachawene kwa maelezo. Pia Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaelekea Wizara ya Nishati, nimwite sasa Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima, Mbunge wa Kawe, aulize swali lake.

Na. 598

**Gesi Asilia Kutumika Kuendesha Magari Nchini**

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakuja na mkakati wa kutumia gesi asilia kuendesha magari nchini ili kuokoa fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mafuta nje ya nchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Judith Kapinga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilikwishaanza programu mbalimbali za matumizi ya gesi iliyogandamizwa *(CNG)* kwenye magari. Mpaka sasa Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imefanikiwa kufungua vituo vitano na inatarajia kufungua vituo vingine vitatu ifikapo mwezi Desemba, 2024. Aidha, jumla ya vituo

16 (vituo mama viwili na vituo vidogo 14) vikijumuisha vituo vinavyohamishika vinatarajiwa kufunguliwa ifikapo mwezi Desemba, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza upatikanaji wa gesi asilia, mwaka 2022 Shirika la Maendeleo ya Petroli *(TPDC)* lilifunga seti tatu za *compressor* zilizoweza kuongeza *pressure* ya futi za ujazo milioni 20. Kwa sasa *TPDC* imeanza utaratibu wa kumpata mzabuni kwa ajili ya kufunga mitambo ya kuongeza mgandamizo wa gesi yenye futi za ujazo milioni 20 kwenye kitalu cha uzalishaji Songosongo. Kazi hiyo inatarajia kukamilika mwezi Machi, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine ili kuhamasisha matumizi ya magari yanayotumia gesi asilia, Serikali inaendelea kutoa msamaha wa kodi kwenye mitungi ya kuhifadhi gesi iliyoshindiliwa kwenye magari na kupunguza ushuru wa magari yanayotumia gesi asilia. Tunaamini mikakati yote hii itachangia kuongeza idadi ya magari yanayotumia gesi nchini itakayopelekea kupunguza uagizaji wa mafuta nje ya nchi na mwisho kuokoa fedha za kigeni, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima, swali la nyongeza.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Serikali nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hii gesi asilia *(CNG)* sasa inatumika kwenye gari nyingi, je, hamuoni kuwa sasa ni wakati mwafaka wa kufungua vituo njiani ili mtu anapokuwa anasafiri kutoka Dar es Salaam kuja hapa kuwe na vituo maalumu kabisa vya gesi asilia ambako mtu anaweza kujaza kwenye gari lake?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima. Ni kweli kwamba Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi tumeanza mkakati wa kutafuta namna ya kuwa na vituo kwa gari

binafsi kuanzia Dar es Salaam mpaka Dodoma kwa awamu ya kwanza. Tayari tumekwishaanza kuwa na mkakati huo na tayari wadau wa sekta binafsi wameshaanza kujitokeza kwa ajili ya kuwekeza kwenye ujenzi wa vituo barabarani kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma. Hata kwa upande wa magari ya Serikali tayari *TPDC* imeanza kuongea na Bohari za *GPSA* ili kuongeza vituo vya *CNG* kwenye hivi vituo vya bohari kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma ili pia hata magari ya Serikali nayo yakiwa yamekwishabadilishwa yaweze kujazwa gesi kutokea Dar es Salaam – Dodoma ambapo ndiyo njia kuu ya magari haya kwa kiasi kikubwa yanapopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa kwa pande zote mbili za magari binafsi pamoja na magari ya Serikali tumekwishaanza kulifanyia kazi suala hili ili kuongeza idadi ya magari ambayo yanatumia *CNG*, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Munira.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kuwa Serikali ina mpango kuwa ifikapo mwaka 2030/2034 wananchi wote wawe wanatumia nishati safi na salama.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha wanasambaza mabomba kwenye nyumba ili ifikapo mwaka 2030/2034 wananchi wote wawe wanatumia nishati safi na salama? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, na nimshukuru Mheshimiwa Munira kwa swali zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Serikali tulikwishaanza awamu ya kwanza ya majaribio kwa ajili ya kuweka miundombinu kwenye maeneo ya Mikocheni pamoja na Mbezi. Aidha, kwa sasa tayari tumeanza mchakato wa kuendelea kuwekeza katika miundombinu hii kwa maeneo mengi zaidi hususan kwa Mkoa wa Dar es Salaam kwanza ili wananchi wengi waweze kutumia gesi

nyumbani, kwa sababu ni ukweli kwamba gesi ya nyumbani kwa miundombinu ina bei nafuu kuliko ile ya mitungi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa tayari mikakati ipo ya kuendelea kuongeza miundombinu nyumbani ili wananchi wengi waweze kutumia gesi nyumbani na tufikie azma ya Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha 80% ya Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Abbas Tarimba.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa juhudi zake za kuleta teknolojia ya gesi katika gari, lakini sasa hivi teknolojia imepanda sana kiasi kwamba kuna magari ya kutumia umeme.

Je, Serikali ina juhudi gani katika kuangalia vilevile uwezekano wa kuhamasisha kuleta magari ya umeme nchini ili kuendelea kupunguza matumizi ya mafuta na gesi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nishukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali inaangalia njia mbalimbali kwa ajili ya kuhamasisha matumizi mbadala, kwa sababu tunaamini ajenda zote hizi zinalenga kwenye kuongeza jitihada za kupambania suala la mazingira. Kwa hiyo, kama ambavyo tunawekeza kwenye nishati ya gesi kwenye magari ndivyo ambavyo tumeshaanza mikakati ya kuweka pia mazingira wezeshi kwa ajili ya kuleta magari yanayotumia umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge jambo hili pia Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kuanzia mwaka jana alishalianza na sisi tunaendelea nalo ili kuhakikisha kwamba tunaweka mazingira wezeshi kwa ajili ya matumizi ya magari ya umeme, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Mohamed Issa.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, hapa katika majibu yake ya msingi Mheshimiwa Naibu Waziri anasema Serikali inahamasisha kwa kupunguza kodi magari ambayo yanatumia gesi, lakini magari yaliyopo nchini ni mengi sana na yanahitaji kutumia gesi. Gharama za ku-*install* mitambo ya gesi kwenye magari ni kubwa sana, ni takribani shilingi milioni 2.5. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba gharama hizi zinashuka?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nishukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama hizi ziko juu kidogo ndiyo maana Serikali tumeendelea kuhamasisha watu wengi zaidi na kampuni nyingi zaidi ziweze kuwekeza katika kuwa na karakana. Tunakubali mwanzo huwa ni mgumu sana, lakini tunakoelekea ni kuzuri kuliko tulikotoka. Mwaka 2021 wakati tunaanza kuhamasisha matumizi ya gesi kwenye magari, kwa wastani tulikuwa tuna-*convert* takribani magari 1,159, leo tunavyoongea tuna magari 5,100 katika mwaka huu wa 2022/2023. Hii ni kwa sababu karakana zimeongezeka kutoka ile moja ya *DIT* hadi nane. Kwa hiyo, wawekezaji wengi wanavyokuja ndivyo ambavyo gharama inavyoendelea kushuka kutokana na ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa tunaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza zaidi na kuja na teknolojia bora zaidi. Tukiwa na karakana nyingi zenye teknolojia ambayo ni bora gharama zitapungua. Kwa hiyo, tunaendelea kulifanyia kazi ili kuhakikisha kuwa gharama hizi zinapungua, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Rehema Migilla.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na kwanza tuipongeze Serikali kwa kuanzisha hii teknolojia ya kutumia gesi kwenye magari yetu, lakini magari mengi yanayotumia hii gesi ni magari ya petroli tu.

Je, Serikali ina mpango upi wa kuhakikisha kwamba magari yanayotumia dizeli nayo yaanze kutumia gesi kwani tunaona Kampuni ya Dangote magari yake yanatumia dizeli, lakini wamefanya *installation* ya mitungi ya gesi, mpango ni upi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tumeanza programu hizi na kwa sasa hivi tulikuwa tuna vituo vitano tu, lakini ili kuelekea kuwa na vituo vingi zaidi tumeanza mazungumzo na hao wawekezaji wa kwenye sekta binafsi ili kuhakikisha wanaona namna ya kuwa na mifumo yote miwili, yaani petroli pamoja na dizeli. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa tunaendelea kulifanyia kazi ili kupata namna ya kuyafanya magari yanayotumia dizeli nayo kuweza kubadilishwa mfumo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa sasa aulize swali lake.

Na. 599

**Hitaji la Chuo cha VETA – Kyerwa**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Chuo cha *VETA* Wilayani Kyerwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa niaba yake, Mheshimiwa Omari Juma Kipanga.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa sasa inaendelea na utekelezaji wa azma ya kujenga chuo cha ufundi stadi katika kila

mkoa na wilaya nchini. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kujenga vyuo vya ufundi stadi katika wilaya 64 kwa wilaya ambazo zilikuwa hazijajengewa vyuo vya ufundi stadi, pamoja na Chuo cha Mkoa wa Songwe. Aidha, Wilaya ya Kyerwa ni miongoni mwa wilaya hizo 64 ambazo zinajengewa vyuo vya ufundi stadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali imekwishapeleka kiasi cha shilingi 324,694,243, pamoja na vifaa vya ujenzi ikiwemo nondo na *cement* kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Chuo cha *VETA* cha Wilaya ya Kyerwa ambapo ujenzi wa chuo hiki upo katika hatua ya ujenzi wa kuta za boma na ufungaji wa *lintel* pamoja na ukamilishaji wa misingi, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Innocent Bilakwate, maswali ya nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na kwanza niishukuru Serikali kwa majibu yake mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wana-Kyerwa wanapenda kufahamu fedha imetengwa tangu mwaka 2022/2023 lakini mpaka sasa hivi ujenzi unaenda kwa kusuasua. Tungependa kujua je, ni kwa nini? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa vifaa vinatoka kwenye Wizara na hii inaweza ikawa sababu ya kuchelesha ujenzi huu, je, kwa nini fedha yote isipelekwe kwenye halmashauri ili ujenzi usimamiwe na halmashauri kama ilivyo miradi mingine kama hospitali za wilaya na vituo vya afya? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, amekuwa akifuatilia ujenzi wa chuo hiki kwa muda mrefu na hata pale Serikali tulipokuwa hatujaanza ujenzi alifuatilia kuhakikisha kwamba chuo hiki kinajengwa kwenye eneo lake, lakini hata tulipoanza ujenzi mwishoni mwa mwaka 2022. Ujenzi huu ulianza mwezi Juni, 2022 ambapo ni mwishoni kabisa mwa mwaka wa fedha, alifuatilia mwenendo pamoja na maendeleo ya ujenzi huu. Kwa hiyo, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa ajili ya ufuatiliaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jambo lake la kwanza kuhusiana na suala la ujenzi kusuasua, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, ni kweli Serikali ilitenga fedha na fedha hii ipo ingawa tunapeleka kule fedha hii kwa awamu. Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba kuna vifaa vile ambavyo tunasema ni *local materials* ndizo hizi ambazo ni shilingi milioni 324 zimepelekwa kule kwa ajili ya ununuzi wa mchanga, maji, mawe na kulipa mafundi ambao wanahudumia kwenye hili eneo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ujenzi huu haujasuasua sana, lakini tunajua kwamba unakwenda taratibu kutokana na ufuatiliaji wa karibu na kuhakikisha kwamba kila kitu kinakwenda sawasawa. Kwa vile ametupa kama ushauri tutahakikisha katika kipindi hiki kifupi tuharakishe ujenzi ule ili Wana-Kyerwa nao waweze kupata chuo hiki kwa ajili ya mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo lake la pili la vifaa kwamba tupeleke kule fedha kule kwa ajili ya vifaa. Nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu, kwa nini tumeamua kununua vifaa hivi kwa kutumia utaratibu wa ununuzi wa pamoja au *bulk purchase*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ununuzi wa pamoja *(bulk purchase)* tumepata faida nyingi sana. Kwanza tumetengeneza *exemption* ya zile kodi kwenye upande wa nondo, *cement* na vifaa vyote vile ambavyo vinatoka viwandani. Kwa hiyo, eneo lile ambalo tulipata *exemption* limetusaidia kwenda kufanya kazi zaidi ya pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushauri wake huu wa kusema tupeleke fedha kule, tutapeleka fedha zile za *local materials,* lakini fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya viwandani tunadhani ni bora tununue moja kwa moja kwa sababu ina manufaa makubwa kuliko tungepeleka fedha hizi zote kule, matumizi yake yangekuwa makubwa na ile *value for money* tungeweza kuikosa, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Cherehani.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Halmashauri ya Ushetu tayari imekwishatenga eneo zaidi ya hekari 42 na lina hati na kila kitu, je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa shule hii ya ufundi katika Halmashauri ya Ushetu?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu swali dogo la Mheshimiwa Cherehani, Mbunge wa Ushetu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Cherehani kwa kutenga eneo lile la Ushetu kwa ajili ya ujenzi wa shule zile za ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilikuwa najibu swali hapa, azma ya Serikali ni kuhakikisha kwamba yale majimbo ambayo hatujajenga Chuo cha *VETA* tutakwenda kujenga shule ya ufundi. Kazi hii tunatarajia ianze mwaka ujao wa fedha wa 2024/2025. Kwa hiyo, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Cherehani na wananchi wa Ushetu, Serikali ya Mama Samia iko kazini na mwezi Julai mwaka ujao wa fedha shule zile 100 za elimu ya amali tutakwenda kuanza ujenzi wake likiwemo na eneo la Ushetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko, nilikuona.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, Wilaya ya Tarime ina halmashauri mbili, Halmashauri ya Wilaya ya Tarime na Halmashauri ya Mji wa Tarime. Halmashauri ya Wilaya ya Tarime tumepata Chuo cha

*VETA*, lakini Halmashauri ya Mji wa Tarime ambayo ni makao makuu ya wilaya hatujapata. Nataka kujua umesema hapo ujenzi wa shule za ufundi utaanza Julai, je, Halmashauri ya Mji wa Tarime nayo inaenda kujengewa hiyo shule ya ufundi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Matiko, kama ifutavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Matiko kwa ufuatiliaji wa karibu kuhusiana na masuala ya elimu na taaluma kwenye mkoa wake pamoja na wilaya zake zote za Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Matiko, azma ya Serikali ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejenga Vyuo vya *VETA* katika wilaya, tunafahamu kwamba kuna wilaya ambazo ni kubwa na zina majimbo zaidi ya moja. Kwa hiyo, kwenye maeneo yote au wilaya zote ambazo zina majimbo zaidi ya moja, tunaangalia ni eneo gani au jimbo gani limejengwa Chuo cha *VETA*. Kule ambako hakujajengwa Chuo cha *VETA* azma ya Serikali ni kupeleka shule ya amali au hizi shule za ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili Jimbo la Tarime Mji lina shule ya ufundi na ni miongoni mwa wilaya au majimbo ambayo ujenzi utaanza mwaka ujao wa fedha, ninashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako.

Tunakwenda Wizara ya Kilimo, sasa nimwite Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum, ili aulize swali lake.

Na. 600

**Ujenzi wa Kongani la Viwanda vya Korosho Lililopo Maranje – Nanyamba**

**MHE. AGNES E. HOKORORO** aliuliza: -

Je, lini kongani za korosho za Maranje Nanyamba zitajengwa ikiwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais alipotembelea Mkoa wa Mtwara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa niaba yake Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa David Ernest Silinde.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Bodi ya Korosho imeanza kutekeleza Mradi wa Kongani ya Viwanda vya Kubangua Korosho katika Kijiji cha Maranje Mkoani Mtwara. Kongani ya Korosho ya Maranje - Nanyamba ni mradi wa kimkakati unaolenga kuongeza thamani ya korosho, kuongeza kipato cha mkulima kwa kuuza korosho zilizoongezwa thamani badala ya kuuza korosho ghafi pamoja na kuongeza ajira katika mnyororo wa uzalishaji wa korosho na mazao yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 10 Juni, 2024 uthamini wa eneo la mradi ekari 1,572 umekamilika ikiwa ni pamoja na ulipaji wa fidia kwa wananchi. Aidha, Serikali imetoa fedha shilingi bilioni 7.5 kwa Bodi ya Korosho kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu katika eneo la ekari 354 kati ya ekari 1,572. Shughuli zilizofanyika mpaka sasa ni kusafisha eneo hilo pamoja na kuanza kwa shughuli za uchimbaji wa visima vya maji na kupeleka umeme katika eneo hilo. Aidha, mkandarasi tayari ameshapatikana kwa ajili ya kutengeneza barabara za ndani kwa kiwango cha changarawe, pamoja na kujenga maghala mawili ya mfano na kiwanda cha kubangua korosho katika eneo hilo. Serikali kupitia Bodi ya Korosho tayari imeanza kuongea na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kujenga viwanda vya kuongeza thamani korosho katika eneo hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnes Hokororo.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, kwanza naomba kuishukuru sana Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kwa kulipa fidia wananchi wa Nanyamba, Maranje na pia kwa kupeleka fedha shilingi bilioni 7.5 kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi. Nina swali dogo tu moja la nyongeza.

Kwa kuwa sasa mradi huo umeanza kutekelezwa na wanawake wa Mkoa wa Mtwara wakiwemo wanawake wa Tandahimba, Newala na Mtwara Vijijini yenyewe ndio wanaobangua korosho kwa sasa kwa kutumia mashine ndogo ndogo.

Je, Serikali imeweka mpango gani wa kuhakikisha hao wanawake wabanguaji wanaotambulika tayari waingie kwenye huo mfumo mara hiyo kongani inapoanza?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Agnes Hokororo kwa kuwatetea wanawake katika mkoa wake na hususani maeneo ya Tandahimba, Mtwara na Newala. Nimthibitishie tu kwamba wanawake wote wanaotokea maeneo yanayozalisha korosho ndio watakaokuwa sehemu ya wanufaika wa mradi huu. Katika mradi ule kuna maeneo ambayo tutatenga ili na wao waweze kuwa sehemu ya mradi huo kwa sababu tunahitaji na wao kuongezewa thamani ya korosho pamoja na kupata kipato, ahsante.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Mimi niipongeze Serikali kwa kulipa fidia kwa wakati na kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Swali langu ni kwamba kwa kuwa mradi ule andiko la awali linasema kutakuwa na ajira rasmi na zisizo rasmi zaidi ya 20,000, je, Serikali imejipangaje katika kupeleka huduma nyingine, hususani huduma za afya, ujenzi wa kituo cha afya pale Maranje, ni lini Serikali itafanya kazi hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najua eneo la Mheshimiwa Mbunge ndilo ambalo tunalifanyia kazi na ameuliza hivi ikiwa ni sehemu ya kuwatetea wananchi katika eneo lake. Nimhakikishie tu katika ule mradi kwenye ile *design* ndani ya ule mradi kuna kituo cha afya. Kwa hiyo, lipo na tutalitekeleza, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tunza Malapo, swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, katika kuelekea utekelezaji wa mradi huo mkubwa na mzuri, nataka kujua Serikali imejifunza nini? Kwa sababu Mtwara kulikuwa na viwanda vya korosho, vingi vimekufa na vimefungwa yaani wakati mnakwenda kutekeleza huo mradi mmejifunza nini ili mradi huo uweze kufanya kazi vizuri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kitu kikubwa ambacho Serikali tumejifunza ni kwamba moja ni kuongeza usimamizi thabiti katika yote ambayo Serikali tunayaanzisha. Sisi kama Serikali tumejipanga kuhakikisha huo mradi unakamilika, tutausimamia na utakuwa endelevu. Haitakuwa ile miradi ambayo tukishaianzisha na baadaye tunaiacha na inakufa. Kwa hiyo, tuamini sisi kwa sababu hili jambo liko ndani ya uwezo wetu, tumekwishalifanyia *studies* za kutosha na litakamilika kwa wakati kama ambavyo tumejipanga.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Katani, swali la nyongeza.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, vile viwanda ambavyo viliuzwa na

Serikali kwa dhamira ya kuendeleza ubanguaji na walionunua viwanda hawakufanya ubanguaji na badala yake wamefanya maghala.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuvirejesha viwanda vile kwa sababu havijafanyiwa kazi iliyokusudiwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, sijui kama liko kwako. Naona ni la Wizara ya Viwanda, lakini kama unaweza kulijibu, lijibu, naona kama unasita, nimemwona Naibu Waziri wa Viwanda.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwanza nishukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo kuhusiana na uongezaji thamani kwenye sekta hii ya korosho. Kimsingi ni kweli viwanda vingi ambavyo vilikuwa vimebinafsishwa wakati ule ambavyo viko kwenye sekta ya korosho, walionunua wengi/waliobinafsishiwa hawakuviendeleza na moja ya anachokisema Mheshimiwa Katani ni kweli na tumeshasema tayari Serikali imeshaanza mchakato wa kuvirejesha viwanda vyote ambavyo viliuzwa au vilibinafsishwa na havifanyi kazi na walionunua hawajaviendeleza. Kwa hiyo, naomba tu watupatie nafasi tukamilishe mchakato huu ili tuvirejeshe Serikalini na kuwatafutia wawekezaji wengine.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni ambao wako ndani ya ukumbi wetu.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni wa Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Mbunge na Naibu Waziri wa Madini, wapiga kura wake kutoka Longido, Mkoa wa Arusha, wasimame tuwaone. *(Makofi)*

Tuna wageni watatu wa Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge na Naibu Waziri wa Kilimo ambao ni viongozi wa madereva wa malori na mabasi ya masafa marefu, karibu sana. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya ambaye ni mkulima kutoka Mkoa wa Simiyu, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Muharami Shaban Mkenge ambaye ni mpiga kura wake kutoka Jimbo la Bagamoyo, Mkoa wa Pwani. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo ambaye ni Daktari kutoka Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma, karibu sana. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi ambaye ni mtangazaji *Azam TV* kutoka Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke ambao ni wadogo zake kutoka Jijini Dodoma, wako pale. *(Makofi)*

Tuna wageni watatu wa Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo ambao ni ndugu wa Wakili Victor Kweka kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wanne wa Mheshimiwa Juma Usonge Hamad ambao ni watoto wake na walezi wao kutoka Jimbo la Chaani, Zanzibar, karibuni sana. (Makofi)

Tuna wageni wanne wa Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhan ambao ni viongozi wa CCM wa matawi kutoka Singida Kaskazini, karibuni sana. (Makofi)

Tuna wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo ambao ni kikundi cha *Family Friends* kutoka Jijii Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni watano wa Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko ambao ni ndugu zake kutoka *Huston Texas,* Marekani wakiongozwa na Mathew Mahono, baba yao pamoja na

wanaye. Tuwaone mko wapi, mmesimama wapi? Karibuni sana kutoka *Texas. (Makofi)*

Tuna wageni saba wa Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka amabo ni wataalamu wa virutubisho lishe kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Tuna wageni 15 wa Mheshimiwa Omar Ali Omar na hawa ni wajasiriamali kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wapo wageni 22 ambao ni Chama cha Wanawake Madereva Tanzania, tuwaone, karibuni sana, inaonesha kuwa wanawake shughuli inabadilika. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 47 na walimu 17 wa Shule ya Msingi Tumaini kutoka Bariadi, Mkoa wa Simiyu, wanafunzi wetu na walimu mko pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 84 na walimu 11 wa Shule ya Msingi Analepo ya Daraja Mbili kutoka Jijini Arusha, karibuni sana watoto wetu. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 48 na walimu wawili wa Shule ya Msingi Amka ya Kigamboni, Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Wabunge anawakumbusha Wabunge wote wa CCM kwamba baada ya kikao hiki kutakuwa na kikao cha *party caucus* mara tu baada ya kuahirisha kikao hiki, pale mnapokutana siku zote. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, sasa nimwite Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Ulyankulu, aulize sasa swali lake.

Na. 601

**Ujenzi Bwawa Kijiji cha Ichemba – Ulyankulu**

**MHE. REHEMA J. MIGILLA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza kutekeleza mradi wa ujenzi wa bwawa katika Kijiji cha Ichemba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imefanya Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa bwawa hilo kati ya mwaka wa fedha 2017/2018 na 2018/2019 ambapo usanifu huo ulijumuisha miundombinu ya bwawa lenye ukubwa wa meta za ujazo milioni 3.6. Ujenzi wa bwawa hilo utakapokamilika utawezesha kumwagiliwa kwa zaidi ya hekta 150 pamoja na kutoa huduma nyingine jumuishi ikiwemo za maji majumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali kupitia Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini *(RUWASA)* Wilaya ya Kaliua itaanza ujenzi wa bwawa hilo litakalohudumia mashamba pamoja na huduma ya maji majumbani. Aidha, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya umwagiliaji ya mashambani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rehema, swali la nyongeza.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu haya yanakatisha tamaa kabisa hasa kwa wananchi wangu ambao wana ndoto kabisa za kutumia hili bwawa, lakini sambamba na hayo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa bwawa hili umekuwa kwenye Ilani ya Uchaguzi kwa awamu mbili mfululizo mwaka 2015 mpaka 2020 limo ikapita bila, lakini mwaka 2020 mpaka mwaka

2025 bwawa hili na lenyewe limo. Ujenzi wa bwawa hili ukikamilika utakwenda kuzisaidia kata zangu tisa na vijiji 27 lakini cha ajabu mpaka leo hivi tunavyoongea hakuna shughuli yoyote iliyoanza kwa ajili ya ujenzi wa bwawa hilo.

Je, hatuoni kwamba kucheleweshwa kwa ujenzi wa bwawa hili siyo tu kwamba unamchonganisha Mheshimiwa Rais na wananchi, lakini pia unaniletea mimi ajali kwa wananchi wangu kwamba siwajibiki kwao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, tumeona miradi mingi ya ujenzi wa maendeleo inapofanyika, wale wananchi wanaozunguka maeneo hayo hulipwa fidia, lakini cha ajabu wananchi wanaozunguka mradi wa hili bwawa hawajafanyiwa hata tathimini juu ya kulipwa fidia au kifuta jasho.

Je, ni upi mpango wa Serikali ili kuwapa kifuta jasho au fidia wananchi hao ambao kwa ridhaa yao wameacha maeneo yao ambayo walikuwa wanafanyia shughuli zao za kimaendeleo ili kuacha mradi ufanyike, upi ni mpango?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, jambo la kwanza nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali haiko hapa kukatisha tamaa wananchi na wala wewe Mbunge kukutengenezea ajali kwa wananchi wako, hiyo siyo wajibu wa Serikali. Jukumu letu sisi kama Serikali ni kuhakikisha tunatatua changamoto kwa wananchi hususani kwenye hili eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge amelitaja la ujenzi wa bwawa, bwawa hili tunajenga kwa ushirikiano kati ya Wizara ya Maji na Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tulishakubaliana kwamba katika eneo lolote ambalo tunajenga bwawa ni lazima Wizara tatu tuhusike ikiwemo Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa maana ya kusaidia wananchi wale hususani wafugaji pamoja na kufuga samaki katika maeneo yale. Kwa hiyo, hizi kazi tunafanya kwa pamoja na ndiyo maana unaweza kuona limechukua muda

mrefu kidogo kwa sababu ni lazima lizingatie Wizara zote tatu katika ujenzi wa aina moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana katika hatua za sasa Wizara ya Maji wako katika hatua za mwisho ili waweze kuja kumtangaza mkandarasi ambaye ataanza ujenzi na sisi Wizara ya Kilimo tutachukua jukumu la kutoa maji katika bwawa na kutengeneza zile *irrigation schemes* kwenda kwenye mashamba ya wananchi, huo ndiyo wajibu wetu ambao sasa hivi tuko katika hiyo hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la fidia hakuna jambo lolote ambalo Serikali tutafanya bila kuzingatia maslahi ya wananchi wa eneo husika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani, nimwite sasa Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mbunge wa Iramba Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 602

**Kukamilisha Ujenzi wa Kituo cha Polisi Nduguti**

**MHE. FRANCIS I. MTINGA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi Nduguti kwa kuwa ujenzi wake umesimama kwa muda mrefu sasa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa niaba yake Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi Nduguti ni Kituo cha Wilaya ya Mkalama kilichoanza kujengwa mnamo mwaka 2015 na kukamilika mwaka 2023 na kuzinduliwa na kwa sasa kinahudumia wananchi wa Mkalama, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa mko wengi kweli, nimewaona wote, lakini tuanze na Mheshimiwa Francis Mtinga.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali kwamba sasa kituo kimeanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo Kidogo cha Polisi cha Ilunda wanafanya kazi zao kwenye kibweni kidogo cha vyumba viwili, Kituo Kidogo cha Polisi Ibaga, wanafanya kazi kwenye Ofisi ya Kijiji, Kituo Kidogo cha Polisi Mwangeza wanafanya kwenye Ofisi ya Kata. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga vituo hivi vidogo ili wenye ofisi zao waendelee na kazi zao kwa sababu wanalalamika sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, polisi wetu ukienda kusikilizwa kesi wanaandika kwenye vikaratasi vya ajabu ajabu tena wanageuza kuangalia mahali ambapo hakuna maandishi. Ni lini Serikali itaanza kusikiliza mambo yetu kwa kutumia TEHAMA ili kuokoa kazi ambazo polisi wetu wanahangaika nazo sana?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji mzuri wa vituo vya polisi kama alivyotaja. Ni maagizo ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhusu ujenzi wa vituo vya polisi vya kata nchi nzima na Wizara yetu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeanza mkakati wa kujenga vituo vya afya vya kata nchi nzima. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge vituo vyako vitatu ulivyovitaja vilivyoko Wilaya ya Mkalama vitaingia kwenye mpango tayari kwa kujengwa katika utaratibu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili la matumizi ya TEHAMA, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Wizara ya Mambo ya Ndani imekwishaanza matumizi ya TEHAMA kwa Jeshi

la Polisi na mwezi uliopita tulizindua hapa Kituo cha Polisi cha Mtumba ambacho tayari kinatumia TEHAMA. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pia jambo hili litafika Mkoa wa Singida hadi Wilaya ya Mkalama kama ambavyo ameuliza, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru, Waheshimiwa Wabunge tumesikia anaongelea vituo vingi viko kwenye bajeti. Kwa hiyo, kama mmoja anaona amekwishajibiwa ningeomba pengine awaachie wale ambao wana maswali ya uhakika. Tutaanza na Mheshimiwa Selemani Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika ilianzisha ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Tanganyika mpaka sasa bado ujenzi hatujapata nguvu yoyote kutoka Serikalini na Serikali iliahidi kutupatia fedha za kuendeleza huo ujenzi.

Je, ni lini Serikali italeta fedha kwa ajili ya kujenga Kituo cha Polisi Wilaya ya Tanganyika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Kakoso, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwapongeze wananchi wa jimbo lake kwa kazi waliyoifanya ya kujenga kituo cha polisi mpaka hatua hiyo waliyofikia. Nimhakikishie kwamba Serikali itaunga mkono wananchi hawa na itatoa fedha ili kumalizia Kituo cha Polisi cha Tanganyika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mama Salma Kikwete.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya ujenzi wa kituo cha polisi katika Kata ya Mchinga?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mama Salma Kikwete, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema nia ya Serikali ni kuhakikisha vituo vya polisi vyote vinakamilika na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Kituo chake cha Mchinga tutazungumza naye ili tuone namna ya kukikamilisha ili kupata huduma za ulinzi na usalama kwa wananchi wake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asia Halamga.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Kituo cha Polisi Kata ya Bassotu, Wilaya ya Hanang umekuwa ni wa muda mrefu sana. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha ili kukamilisha ujenzi wa kituo hicho?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asia Halamga, Mbunge wa Vijana, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi Bassotu kimetengewa fedha katika mwaka wa fedha 2024/2025 ili kuweza kukamilika na kutoa huduma kwa wananchi wa Bassotu na Wilaya ya Hanang kwa ujumla.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dorothy Kilave.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ya kutujengea vituo vya polisi, lakini Kituo cha Polisi Chang'ombe ni cha Kimkoa wa Kipolisi Dar es Salaam. Je, Serikali mna mpango gani wa kujenga Kituo cha Polisi cha Tandika ndani ya Jimbo la Temeke?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kilave, Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea maombi ya ujenzi wa Kituo cha Polisi Tandika kama alivyosema na tuweke kwenye mpango na kutengewa fedha ili tuweze kujenga kituo cha polisi kwa ajili ya ulinzi na usalama wa wananchi wa Temeke.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rwamlaza.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kuniona, wananchi wa Kata ya Kasharunga katika Kijiji cha Kasharunga katika Wilaya ya Muleba wamejenga Kituo Kidogo cha Polisi na kimekamilika. Ni lini Serikali itafungua kituo hicho kwa kupeleka askari ili wananchi waweze kupata huduma waliyoihitaji?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu swali la Mheshimiwa Rwamlaza, kwanza nichukue nafasi hii kuwapongeza kwa ujenzi wa kituo cha polisi katika eneo hilo na nimhakikishie kwamba tuko tayari kwenda kufungua wakati wowote hata baada ya Bunge la Bajeti na tutaleta askari tayari kwa kutoa huduma katika eneo hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suma Ikenda.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na ujenzi wa vituo vya polisi, Mbarali, Kyela, Chunya na *Mbeya DC*, askari polisi hawana nyumba za kuishi, wao wanaishi uraiani yaani wamepanga. Je, ni lini Serikali itawajengea nyumba askari polisi hao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Suma, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikijenga nyumba za polisi katika maeneo mbalimbali kwa awamu na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika maeneo ambayo ameyataja katika Wilaya ya Chunya, Mbarali na maeneo mengine tutatenga fedha kwa ajili ya kujenga nyumba za polisi katika maeneo hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtaturu, swali la nyongeza.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Kata ya Mkiwa tumeanza ujenzi wa Kituo Kidogo cha Polisi ambacho ni kituo cha kimkakati. Mimi kama Mbunge nimechangia shilingi milioni tano kutoka katika mfuko wa jimbo na wananchi wameji-*organize* na wadau. Ni lini Serikali itatuunga mkono ili kumalizia kituo hicho kwa ajili ya usalama wa wananchi wetu?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mtaturu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imetenga shiliongi bilioni 3.8 kwa ajili ya kumalizia maboma yote 77 yaliyojengwa na wananchi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge baadaye tuonane pengine kituo chake alichokitaja kiko kwenye maboma haya 77 ili tuweze kukimalizia katika mwaka wa fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fiyao, kwa kifupi.

Wabunge naomba muulize kwa kifupi sana.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua ni upi mpango wa Serikali wa kujenga kituo cha kisasa katika Mji wa Tunduma ili kiendane na mahitaji hasa ukizingatia ni lango kuu la *SADC*?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella Fiyao, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba maeneo yote ambayo yana *population* kubwa, lakini pia yana maeneo makubwa ya biashara kama Tunduma, yanakuwa na vituo vya polisi vya uhakika ili kulinda usalama wa wananchi na mali zao. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge eneo hilo pia tumelichukua, tulipange kwenye mpango, ili tuweze kujenga kituo cha polisi cha kisasa kama ambavyo ameomba Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nicodemas.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri, Kata ya Masumbwe tayari tuna eneo la kituo cha polisi, lakini pia mimi kama Mbunge kule Lulembela nimetoa shilingi milioni tatu, Gilorwanguru nimetoa mifuko 100 kwenye kituo cha polisi. Je, ni lini Serikali Kuu mtatupa *support* Mbogwe kuweza kukamilisha vituo hivi vya polisi vilivyopo?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nicodemas Maganga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye baadhi ya majibu ni kwamba Serikali imetenga fedha kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kumalizia maboma yote ambayo wananchi wameshaanza kujenga, yapo maboma 77. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge tuonane baadae pengine kituo chako pia kama kipo kwenye vile 77 kitatengewa fedha ili kumalizia kazi kubwa waliyofanya wananchi wa Mbogwe, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Liwale pamoja na kwamba haina Kituo cha Polisi cha Wilaya chenye hadhi, lakini kuna uhitaji mkubwa sana wenye Tarafa ya Kibutuka, Lilombe na Kimambi na ni ahadi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini vituo hivi mtakuja kuvijenga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kuchauka, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema Serikali imepanga kujenga vituo vya polisi vya kata kwa awamu. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge pia kata zake alizotaja naamini zipo kwenye mpango, kwa hiyo, tutazitengea fedha ili ziweze kujengwa na wananchi wapate ulinzi na usalama wa mali zao, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oliver.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, Kyerwa ni Wilaya mpya lakini mpaka sasa hakuna kituo cha polisi. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kituo cha Polisi katika Wilaya ya Kyerwa?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oliver Daniel, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na ujenzi wa vituo vya kata, kama nilivyosema Serikali inaendelea kujenga vituo vya wilaya kwa kupitia Mfuko wa Tozo na Tuzo. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Wilaya ya Kyerwa ni moja kati ya wilaya za kimkakati kwa hiyo, tutajenga kituo cha polisi katika wilaya hiyo, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Usonge, swali la nyongeza.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi kilichokuwepo pale Mchangani kwenye Jimbo langu la Chaani ambacho kwa takribani 80% kimeshatengenezwa na wawekezaji? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Usonge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana kwa ujenzi wa kituo ambacho kimefika 80% na ninamhakikishia Serikali kwa kazi hiyo nzuri iliyofanywa na wananchi, 20% iliyobaki tutamalizia katika mwaka wa fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Katika Kata ya Bukumbi wananchi na Mbunge tumejenga kituo kizuri cha afya. Lini Serikali itapeleka magari au pikipiki, kwa ajili ya usafiri wa hawa askari?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani alikuwa anaulizia swali kituo cha polisi na siyo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maige, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali mpaka sasa imetoa pikipiki 105 kwa ajili ya vituo vya polisi katika maeneo mbalimbali nchini na kwa jinsi ya upatikanaji wa fedha, Serikali itatoa pikipiki kwa ajili

ya kuhudumia vituo vya kata, kama alivyotaja Mheshimiwa Mbunge Maige.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maryam Mwinyi.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Kijiji cha Pujini kilichopo Wilaya ya Chakechake, Mkoa wa Kusini Pemba ni kijiji ambacho kina matukio ya uhalifu siku hadi siku, je, ni lini Serikali itajenga kituo hicho?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Mwinyi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, Serikali ina mkakati wa kujenga vituo vya kata nchi nzima, nadhani takribani kata 4,434 zimebaki. Kama nilivyosema, vinajengwa kwa awamu, havijengwi mara moja, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kituo alichotaja kitawekwa kwenye mpango ili kiweze kutengewa fedha kwa miaka inayokuja na kujengewa kituo cha polisi katika eneo lake, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tutamaliza na Mheshimiwa Neema na Mheshimiwa Priscus Tarimo.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuiuliza Serikali, kituo cha polisi kilichopo Kata ya Kashai kimepewa chumba kimoja katika Ofisi ya Kata na tukizingatia kwamba Kata ya Kashai ndani ya Jimbo la Bukoba Mjini ina wakazi zaidi ya 33,000. Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi kwenye Kata ya Kashai? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema Lugangira, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua Kata ya Kashai ina wananchi wengi, kama alivyotamka Mheshimiwa Mbunge, kwa hiyo namhakikishia kwamba kwa kuwa ina wananchi wengi na pia kunakuwa na hatari ya kuwa na wizi au matukio mbalimbali. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa kata yake aliyoitaja ya Kashai na yenyewe tumeichukua na tutaiingiza kwenye mpango kwa ajili ya kujengewa Kituo cha Polisi, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Priscus Tarimo.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Karanga, viongozi pamoja na wananchi wamejenga kituo kizuri sana cha polisi, lakini bado hakijakamilika na mimi nimewasaidia tofali 2,000. Je, Waziri yuko tayari kuja kukitembelea na ku-*allocate* bajeti ya kumalizia?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa aliyofanya ya kujenga Kituo cha Polisi katika Kata aliyoitaja ya Karanga. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge niko tayari kwenda kwenye kituo hicho kukikagua na kukitengea fedha, kwa ajili ya kumalizia kazi kubwa waliyoifanya wananchi wa Karanga, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunakwenda Wizara ya Maji na namwita Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 603

**Kukamilisha Mradi wa Maji Mpasa King'ombe, Nkasi**

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha mradi wa maji uliopo Mpasa, King'ombe, Kata ya Kala, Wilayani Nkasi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa niaba yake Naibu Waziri - Mheshimiwa Andrea Mathew Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha Miradi ya Maji ya Mpasa na King'ombe, Wilayani Nkansi, Mkoa wa Rukwa na inatoa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi. Kwa sasa skimu hizo zinasimamiwa na chombo cha Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii *(CBWSO)* cha Chipiruka kwa ajili ya uendeshaji na matengenezo. Skimu hizo zinahudumia jumla ya watu 11,267 waishio kwenye vijiji vitatu vya King'ombe, Mpasa pamoja na Mlambo kupitia vituo 42 vya kuchotea maji, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali na ninaipongeza, kama imemaliza kutengeneza mradi huo, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan amenunua magari/mitambo ya kuchimbia visima kila mkoa. Napenda kujua ni kwa nini sasa Mji Mdogo wa Namanyere bado hawajachimbiwa visima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Bwawa la Maji la Mji Mdogo wa Namanyere ni muhimu sana kwa Wilaya ya Nkasi. *RUWASA* wamejipangaje kumaliza ujenzi wa Bwawa la Maji la Mji Mdogo wa Namanyere? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Rukwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge, ameendelea kuwa msemaji mkuu wa wanawake wa Mkoa wa Rukwa kuhusiana na suala la maji, nakupongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa hili swali inawezekana likaulizwa na Waheshimiwa Wabunge wengi kuhusu mitambo ambayo Mheshimiwa Rais ameinunua. Mitambo hii iliponunuliwa ni kwamba hatukuwa tumejiandaa na wataalamu wa kuiendesha, matokeo yake mitambo hii imejikuta kwamba ikienda katika maeneo ya porini inakwama na wataalamu wetu wakawa bado hawajaiva kiutaalamu kiasi kwamba ikawa inaleta changamoto sana, lakini kwa sababu hiyo, Mheshimiwa Waziri, Juma Aweso, alielekeza wataalamu wetu wapatiwe mafunzo toshelezi ili waweze kuiendesha mitambo hii na kufanya kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuhakikishia na Bunge lako Tukufu kwamba tayari Mheshimiwa Waziri ametoa mwongozo na kwa mwongozo huo sasa tunaenda kuanza uchimbaji wa visima kwa kutumia hii mitambo ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa fedha nyingi sana kuinunua. Sasa inaenda kuanza kufanya kazi kwenye vile visima vitano vitano vya kila Mbunge ambavyo ni visima 900. Kwa hiyo, nakuhakikishia na Bunge lako kwamba mitambo hii sasa iko tayari kuingia kazini na kuweza kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuhusu Bwawa la Namanyere, Mheshimiwa Waziri ametoa maelekezo ya kutoa fedha takribani shilingi milioni 400 mwishoni mwa mwezi wa nne na tayari kweli, kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema zimeshatolewa na zimeshafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaelekeza *RUWASA* kuhakikisha kwamba bwawa hili sasa linaanza kufanyiwa kazi kwa uharaka zaidi ili liweze kutoa mahitaji ambayo yametarajiwa na kutatua changamoto ya maji katika maeneo ya Namanyere, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yawe mafupi kwa watakaopata nafasi. Tuanze na Profesa Patrick Ndakidemi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa furs ana naishukuru Serikali kwa shilingi milioni 500 ambazo zilikwenda kujenga mradi kwenye Kata ya Kimochi katika Vijiji vya Mdawi, Shia, Sango na Kisaseni, lakini havijapata maji. Je, Serikali ina mpango gani wa kutusaidia kupata maji katika vijiji hivi?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Serikali ilitenga shilingi milioni 500 na hasa katika bajeti hii ya mwaka 2024/2025 tumetenga fedha nyingine za kwenda kuhakikisha kwamba tunaenda kumalizia vijiji ambavyo vimebaki kufikishiwa huduma ya maji ambavyo ni Vijiji vya Sango, Mdawi pamoja na Shia. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwa sababu imekuwa ni ndoto yake kuhakikisha kwamba vijiji hivi vinapata huduma ya maji safi na salama, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida Khenani.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Waziri hilo Bwawa la Mamlaka ya Mji Mdogo wa Namanyere bajeti iliyotengwa ni shilingi bilioni 6.7, fedha iliyoenda ni shilingi milioni 950, leo tunazungumza ni tarehe 12 Juni, tunaenda kumaliza mwaka wa bajeti na mpaka sasa mkataba tu haujasainiwa. Ni upi mkakati wa Serikali ambao upo kuhakikisha hizi fedha zinakwenda na huu mradi unakamilika?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua changamoto ya bwawa hili na ninatambua kwamba wananchi wake wanasuburi kuona nini kinafanyika na kwa bahati nzuri pia Mheshimiwa Mbunge uliuliza kuhusu hili swali na nikakupa mkakati wa namna gani tunaenda kufanya. Naomba uwe na subira kwa sababu miradi hii inafanyika kwa hatua na mkandarasi akishapewa mkataba maana yake ni kwamba tutaanza kwa kumlipa *advance,* hatumlipi pesa yote, maana yake ni kwamba pesa nyingine itakayofuatia ni kulingana na ambavyo atakuwa ana *raise certificate* kulingana na *progress* ya kazi ambayo atakuwa anaifanya. Kwa hiyo, nakutoa wasiwasi, Serikali inatambua na tunaenda kulifanyia kazi kwa ukamilifu, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti Majala.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, Mheshimiwa Naibu Waziri ulifika Kata ya Soya, Kijiji cha Mbarada na ukakutana na wananchi na wakakueleza kilio chao cha uhaba wa maji, ukawaahidi upatikanaji wa maji haraka iwezekanavyo. Ni lini unapeleka mitambo hiyo Kijiji cha Mbarada ili waweze kupata maji safi na salama kwa wakati?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kunti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sikosei Kijiji cha Mbarada kiko Wilaya ya Chemba na katika maeneo ambayo tulisikitishwa sana kama Serikali, baada ya kukuta hali ya upatikanaji wa maji ambayo wanayatumia wananchi wa pale yalikuwa mabaya sana, lakini napenda nimpe taarifa kwamba baada ya ile ziara na mpaka sasa, tukimaliza kipindi cha Bunge hapa, naweza nikakuonesha mitambo imeshafika pale na maji tayari wameshaanza kuona namna ambavyo yanatoka. Tunaamini kwamba uchimbaji na usambazaji wa miradi ya maji una hatua,

kwanza kupata chanzo, kutengeneza tenki, kujenga mtandao na baadae kutengeneza maeneo ya kuchotea maji. Kwa hiyo, mradi huu utakamilika na wananchi watapata huduma ya maji, ahsante sana.

**MWENYEKITI;** Ahsante, ameelewa. Mheshimiwa Dkt. Jeremiah Amsabi.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, katika Wilaya ya Serengeti Miradi ya Maji ya Gesaria, Nyamititा, Rigicha na Nyiberekera imekwama kabisa. Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa miradi hii?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Serengeti katika eneo la Nyamitita, tayari mkandarasi wetu yuko *site,* yuko kwenye utengenezaji wa *line* ya umeme ya kilometa sita. Pia katika eneo la Rigicha mkandarasi tayari yuko katika eneo na anaendelea kurekebisha *line* ya umeme, lakini katika kijiji ambacho amekitaja, jina lake naomba liingie kwenye *Hansard* kama alivyolitaja, kuna visima, vituo 30 vya kuchotea maji tayari vimekamilika na asubuhi hii *DM* alikuwa katika eneo hilo na amenipatia mrejesho wa kazi ambayo imeshafanyika.

Kwa hiyo, namtoa hofu Mheshimiwa Mbunge kazi inaendelea na tutahakikisha kwamba maji yanapatikana kwa usahihi zaidi, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, pale Bunda tuna mradi wa maji kutoka Nyabihu umekamilika, lakini kuna changamoto ya miundombinu na ninyi Serikali moja ya changamoto ambayo mnakabiliana nayo ni upotevu wa maji. Kuna bomba kubwa kutoka Butakale, Kata ya

Bunda Stoo, unaenda Kasakwa kule kwenye tenki, Mlima Balili, inahitajika shilingi bilioni 1.7 kujenga lile bomba ambalo ni chakavu kuokoa maji yasipotee ili wananchi wa Bunda Mjini wapate maji safi na salama. Lini sasa mtatoa hizo shilingi bilioni 1.7 kwa ajili ya ujenzi wa bomba kuu?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mheshimiwa Bulaya kama Serikali tukushukuru kwa kutupatia taarifa kama hiyo. Ni mkakati wa Serikali kuendelea kuboresha miundombinu chakavu yote ambayo inatusababishia kuwa na upotevu wa maji kwa sababu tunayazalisha kwa gharama na yanapokuwa yanapotea maana yake ni kwamba Serikali inaingia kwenye hasara kubwa.

Kwa hiyo, nakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge nalipokea hilo na nitaenda kulifuatilia ili tuone tunafanya nini kuhakikisha kwamba bomba hilo linaenda kujengwa, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Cosato Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri alifanya ziara katika Halmashauri ya Mji wa Mafinga. Wananchi wa Itimbo wanauliza, mkandarasi ameshapatikana, ni lini anaenda kuanza kazi katika Kijiji cha Itimbo?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa swali zuri. Mheshimiwa Mbunge kwa kweli tunaendelea kushirikiana vizuri na mkandarasi na ataingia *site* baada ya mwaka wa fedha kuanza, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mhata.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nanyumbu kwenye Kata ya Maratane mwaka jana, mwezi Julai tuliingia mkataba na mkandarasi wa kusambaza maji katika kata hiyo. Hadi sasa hivi mkandarasi hajaanza kazi, sababu kubwa hajapata *down payment.*

**MWENYEKITI:** Swali.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali, ni lini atapata *advance* ili aanze kazi?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongee kidogo kwenye suala hili.

**MWENYEKITI:** Kwa kifupi kwa sababu majibu unaweza kuwa umeyasema.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na changamoto na wakandarasi, ni kweli kabisa kuna wengine hawajapata *advance payment,* lakini wengine hata kufanya ile *mobilization* hawajafanya, kwa hiyo, inatutia wasiwasi kuanza kuwalipa wakati hata *mobilization* ambayo iko kwa mujibu wa sheria kwamba tayari ukishapata mkataba unatakiwa kuanza kufanya *mobilization.* Kazi ambayo tunaifanya sasa hivi ni kuwasisitiza wakandarasi wote ambao tumeingia nao mikataba kuanza kufanya *mobilization,* tuone *commitment* yao na Serikali itatoa fedha kwa ajili ya *advance payment* kuhakikisha kwamba miradi inaanza kutekelezwa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Michael Mwakamo.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Boko, pale Mnemela, Jimboni Kibaha Vijijini kuna tatizo la maji la muda mrefu na wananchi wamechoka kuona mabomba ambayo watu wa *DAWASA* wanashindwa kuyafanyia kazi. Je, Waziri unatoa agizo gani kwa Meneja wa *DAWASA* ili aweze kukamilisha mradi ule na watu wa Boko wapate maji?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa changamoto hii naomba nitumie fursa hii na Bunge lako Tukufu kumwelekeza Mkurugenzi Mtendaji wa *DAWASA* kwenda kulifanyia kazi eneo hili na kuweza kufanya tathmini, kujiridhisha ukubwa wa tatizo ili Serikali iweze kuchukua hatua na wananchi waendelee kupata huduma ya maji safi na salama, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tumalize suala la maji. Namuita sasa Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, aweze kuuliza swali lake.

Na. 604

**Usambazaji wa Maji Safi katika Wilaya ya Meru**

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatenga fedha kumalizia usambazaji wa maji safi na salama Kata ya King'ori, Wilayani Meru hususani katika Vijiji vya Meru kwa Philipo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Maleu, eneo la kwa Philipo, Kata ya King'ori, Wilayani Meru kinapata huduma ya maji safi na salama kupitia Skimu ya Maji ya Makilenga ambayo kwa sasa haitoshelezi mahitaji kutokana na kuhudumia vijiji 22 vyenye mahitaji ya jumla ya lita 4,931,000 za maji kwa siku wakati uzalishaji ukiwa lita 2,465,500 kwa siku. Katika kuboresha huduma ya maji katika kijiji hicho, Serikali katika mwaka wa fedha 2024/2025 itashirikiana na Shirika la *Korea International Cooperation Agency (KOICA)* kutekeleza mradi wa usambazaji maji safi na salama katika vijiji sita kikiwemo Kijiji cha Maleu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zitakazotekelezwa katika mradi huo ni pamoja na ujenzi wa vyanzo vya maji na uboreshaji wa mitambo ya maji. Muda wa utekelezaji wa mradi huo ni miezi 18 ambapo kukamilika kwake kutanufaisha wananchi wapatao 16,584 waishio katika vijiji sita vya Maleu, Oldonyongiro, Shambarai Burka, Msitu wa Mbogo, Sakina Chini na Sakina Juu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Serikali na nitumie nafasi hii kuishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu mpendwa kwa juhudi kubwa ambayo tunaiona jimboni ya kutaka kumaliza kabisa tatizo la maji. Tunavyozungumza sasa hivi mtambo wa kuchimba maji visima virefu kwa ajili ya kufuata maji ya ardhini huko jimboni na kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo kuna shida kubwa sana ya maji katika Tarafa ya King'ori ambayo imebeba Kata za Kikatiti, Majengo, Malula, King'ori, Maruvango, Leguruki, Ngarenanyuki, Uwiro na Ngabobo. Pia eneo hilo maji yana-*fluoride*...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, swali.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu, je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza changamoto hizi za maji eneo hilo? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kuona Mheshimiwa Mbunge anatambua kazi kubwa ambayo inafanywa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na kweli mtambo upo na kama ambavyo nilijibu

katika majibu mengine, mitambo hii sasa wataalamu tayari wameshapatikana wanaingia *site* kuhakikisha kwamba visima vinaanza kuchimbwa. Pamoja na hilo, Skimu ya Makilenga inahudumia takribani 50% ya Tarafa ya King'ori. Kwa hiyo, tumwombe Mheshimiwa Mbunge tuendelee kushirikiana kuhakikisha kwamba changamoto hii inaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa sasa pia Serikali inashirikiana na mdau wa maendeleo kutoka Korea kuhakikisha kwamba kuna madini ya *fluoride* katika eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge ameongelea na madini hayo sasa tunaenda kufanya mchakato wa kuyaondoa na kuchuja na kuhakikisha kwamba wananchi wa eneo lile wanapata maji ambayo hayatokuja kuwa na madhara katika afya zao. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, Serikali tayari imeshaanza kufanya kazi hiyo, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunamalizia na Wizara ya Maliasili na Utalii, muda wetu umekwisha. Sasa namwita Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, aulize swali lake.

Na. 605

**Mgogoro wa Ardhi Kati ya *TANAPA* Kitulo/*TFS* na Wananchi**

**MHE. ORAN M. NJEZA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamaliza mgogoro wa muda mrefu wa ardhi kati ya *TANAPA* Kitulo/*TFS* na wananchi wa Kata za Ilungu, Igoma na Inyala?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa niaba yake Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Kamati ya Usalama ya Wilaya ya Mbeya Vijijini na uongozi wa kata zilizopakana na Hifadhi ya Taifa ya Kitulo imefanya mikutano 15 kati ya tarehe 17

Mei, 2023 na tarehe 9 Novemba, 2023. Mikutano hiyo ililenga kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa uhifadhi, dhana ya ujirani mwema na kuwashirikisha wananchi katika juhudi za pamoja za kutambua mipaka ya hifadhi kwa faida za hifadhi, jamii na Taifa kwa ujumla. Kufuatia mikutano hiyo, mgogoro huu umemalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza mahusiano mema na jamii zinazozunguka hifadhi, Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia *TANAPA* kwa kushirikiana na Serikali ya Mkoa wa Mbeya imepanga kuweka vigingi kwenye mpaka wa hifadhi kwa umbali wa kilometa 82 katika mwaka wa fedha 2024/2025 ili kurahisisha utambuzi wa mipaka ya hifadhi na vijiji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oran Manase Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na pia nashukuru kwa majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa maeneo yaliyotajwa yanatumiwa na wananchi wa kata hizo kwa kilimo kwa karne kadhaa na hawa wananchi wamekuwa vinara wa kutunza mazingira na kwa uthibitisho hao viongozi wawili wa kimila walitambulishwa hapa Bungeni wiki iliyopita kulipokuwa na maadhimisho ya kutunza mazingira.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari sasa akatembelee hayo maeneo akaongee na wananchi na vilevile pamoja na kutatua mgogoro ambao haujaisha akawapongeze kwa ajili ya kutunza mazingira? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa vile hawa wananchi wamekuwa vinara wa kutunza mazingira na wamefanya vizuri sana na kiasi kwamba wao ni walinzi wazuri kuliko hata hao askari.

Je, Wizara haioni umuhimu wa kuanza kushirikiana na wananchi kutoa misaada ya *CSR* kwa ajili ya kuwashirikisha ili kuwapa motisha ya kutunza mazingira? Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la kwanza, niko tayari kwenda kutembelea eneo hili ili tuweze kufanya hayo ambayo ameeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali la pili, Wizara kupitia taasisi zetu tuna mipango ya ujirani mwema kwa wananchi wanaozunguka kwenye maeneo ya hifadhi zetu. Niwaagize wataalamu wetu walioko uwandani waende kwenye maeneo yanayozunguka hifadhi hii ili wakafanye kazi ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu uibuaji wa miradi ya kijamii ili hatimaye miradi hiyo iweze kupata ufadhili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza. Tutampa swali mtu mwingine kama huwezi.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itamaliza mgogoro wa mpaka kati ya Pori la Akiba la Selous na Kijiji cha Mtepela? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utatuzi wa migogoro ni mchakato na tunavyozungumza kuna mchakato wa utatuzi unaendelea. Namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira tukamilishe kazi ile ili tuweze kuondokana na changamoto hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itamaliza mgogoro uliopo katika Kitongoji cha Isela, Kijiji

cha Ndolezi na eneo la Kimondo kati ya wananchi na Ngorongoro?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye swali lililopita, utatuzi wa migogoro ni mchakato naomba tutoe fursa kwa Serikali iweze kushughulikia migogoro hii ili iweze kumalizika.

**MWENYEKITI:** Tutamaliza na Mheshimiwa Bahati.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, mgogoro kati ya *TFS* na Kijiji cha Kapyo, Kata ya Mahongole, Wilaya ya Mbarali tayari ulishamalizika baada ya wataalamu wa *TFS* wa Kanda kukaa kikao cha pamoja na wataalamu wa halmashauri pamoja na wanakijiji. Kinachosubiriwa kutoka Wizarani ni barua ambayo itawaruhusu sasa wale wanakijiji kuendelea na shughuli zao. Ni lini sasa tutapata hiyo barua ili kijiji hiki kiendelee na shughuli zake? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuuagiza uongozi wetu wa *TFS* kwa haraka sana uweze kutoa barua hiyo ili kumaliza jambo hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa maswali kwa siku ya leo. Nina wageni ambao wako ndani ya ukumbi wetu na ningependa tuwafahamu na tuwatambue.

Kuna wageni 34 wa Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani na hawa ni Makatibu Kata CCM kutoka Tandahimba, Mkoa wa Mtwara wakiongozwa na Ndugu Said Mtopa, Katibu wa Jumuiya ya Wazazi Wilaya ya Tandahimba, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni 39 na hawa ni wageni wa Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, hiki ni Kikundi cha Wafugaji kutoka Wilaya ya Rungwe, Mkoa wa Mbeya, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni 106 wa Mheshimiwa Anna Lupembe na hawa ni wachungaji kutoka Kenya, Uganda, Rwanda na Ujerumani. Wapo kwenye Jiji la Dodoma wakiendesha Semina ya Neno la Mungu, karibuni sana wageni wetu kutoka *East Africa* na kutoka Ujerumani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nawakumbusha kwamba Katibu wa CCM anawakumbusha kwamba *party caucus* itaendelea mara tu baada ya kikao hiki kwenye ukumbi ule ule ambao mnaufahamu.

Tumefika mwisho wa shughuli ya leo na sasa naahirisha Bunge hili mpaka kesho tarehe 13 Juni, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 13 Juni, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*